

# رَفَقًا أَهْلَ السُّنَّةِ بِأَهْلِ السُّنَّةِ

## NASWAHA YA SHAYKH ABDUL-MUHSIN AL-ABBÂD KWA WANAFUNZI WA KI'ILIMU (T WALABATUL 'ILM)

Katika vitabu vilivyo na umuhimu watu kuvisoma vya Wanavyuoni tulionao sasa ni ; *Majmoo'al-Fataawa* cha Sheikh wetu, Imaam wa Watu Wa Sunnah katika zama zake, Sheikh Ábdul-Ázeez bin Ábdillaah bin Baaz; Fataawa [za Saudi Arabia] kamati ya kudumu katika taaluma za utafiti na hukumu; maandishi ya Sheikh wetu, al-állâmah, Sheikh Muhammad al-Amin ash-Shanqîti - hususan *Adhwâ' ul-Bayân fi Ídhwâh al-Quráni bil Quráni*; na maandishi ya wanavyuoni wawili vigogo, Sheikh Muhammad bin Sâlih al-Úthaimîn na Sheikh Muhammad Nâsir ad-Dîn al-Albâni ((رحمهم الله)).

Vilevile ningelipenda kuwanaswihi wanafunzi wa ilimu katika kila mji wafaidike na wenye kujishughulisha na ilimu miongoni mwa Watu Wa Sunnah walio kwenye sehemu zao; kama wanafunzi wa Sheikh al-Albâni walioko Jordan walioasisi Markaz baada ya kufa Sheikh wao kwa jina lake<sup>1</sup>; kama Sheikh Muhammad al-Maghrawi aliyoko Morocco, Sheikh Muhammad Áli Farkus na Sheikh al-Íd Sharîfi aliyoko Algeria, na wengineo miongoni mwa Watu Wa Sunnah. Kutokamana na naswiha kwa Watu Wa Sunnah ni kwamba yoyote miongoni mwao atakaefanya makosa na atanabahishwe katika makosa yake, wala asifuatiliwe kwa makosa yake. Watu wasimuepuke kwa sababu ya kosa lake, bali wachukuwe faida kutoka kwake, hususan iwapo hatopatikana yule ambae atakaekuwa ni bora kuliko yeye katika Ilmu na fadhla.

Nawausia vijana watahadhari na kujishughulisha kuandama makosa ya wanafunzi wa wanavyuoni na kupoteza wakati wao kuifuatilia mitandao ya internet zenye kujihusisha na ukusanyaji wa makosa yao na kuonya watu dhidi yao kwa sababu ya [kukosea huko]. Sheikh Muhammad bin Suleiman al-Ashqar alikosea makosa makubwa kwa kumtukana Swahaba Abi Bakrah (رضي الله عنه) na riwaya zake, na [katika]

<sup>1</sup> [Mf]Yaani; Sheikh Áli Hasan al-Halabi, Sheikh Mash-hoor Hasan Aal Salmân, Sheikh Muhammad Musa Nasr Ál-Nasr, Sheikh Husain bin Áwdah al-Áwâishah, Sheikh Salim bin Éid al-Hilâli na wengineo.

kujihusisha kwake<sup>2</sup> na masála ya mwanamke kutawala na kushirikiana na wengine katika utawala. Nikamrudi katika kitabu kwa jina, *ad-Difaa' án as-Sahaabi Abi Bakrah wa Marwiyaatihi wal-Istidlaal li Man' Wilaayah an-Nisaa' álaar-Rijaal*<sup>3</sup>, na nilipowatahadharisha watu na makosa yake mabaya sikuwa ni mwenye kutahadharisha watu wasisome vitabu vyake vyenye faida; miongoni mwa wapokezi wa swahîh mbili, na vilevile [vitabu] vyengine, kuna wapokezi wenye kusifika na bidáh na riwaya zao zimekubaliwa licha ya kutolewa ilani na wanavyuoni kuhusu bidáh hizo kwa ajili ya kuwazindusha watu dhidi ya watu hao.

[Mf]: Mfasiri

Imefasiriwa na Muhammad Awadh Salim Basawad

[www.qssea.net](http://www.qssea.net) [MOMBASA, KENYA]

---

<sup>2</sup> [Mf]Yaani; Sheikh Muhammad bin Suleimaan al-Áshqar

<sup>3</sup> [Mf]Yaani; *Kumtetea Swahaba Abi Bakrah Pamoja Na Riwaya Alizozipokea, Na Dalili Za Kuzuiya Kutofaa Kwa Mwanamke Kuwa Na Usimamizi Juu Ya Mwanamume.*